

OFISI YA WAZIRI MKUU TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

Anuani ya Simu:
Simu:
EMAIL:



Arusha Girls High School,
S.L.P. 16034,
ARUSHA.

Unapojibu tafadhali taja:
Kumbukumbu Namba: AGHS/F.5/2015

1 JULAI 2015

MZAZI WA
S.L.P.

**PICHA P/S YA
WAZAZI NA
MTOTO**

YAH: **MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE KIDATO CHA TANO**

- 1.0 Ninayo furaha kukujulisha kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na shule ya Arusha Girls High School Kidato cha TANO (V) mwaka 2015/2016.
- 2.0 Umechaguliwa /umekubaliwa kuchukua masomo ya

EGM

PGM

- 3.0 Shule hii ni ya wasichana tu na wataishi Bweni.
- 4.0 Shule itafunguliwa siku ya tarehe saa tatu asubuhi hadi saa kumi 10.00 jioni.

NB Shule iko Halmashauri ya jiji la Arusha kata ya Olasiti. Ukifika Arusha mjini, shule iko KM 2.5 kutoka barabara kuu iendayo Kisongo/Monduli kusini mwa uwanja wa ndege Arusha.

- (i) Mwanafunzi alete vifaa vyote kama ilivyoagizwa hapo chini. Malipo yote ya ada na michango mingine yafanyike kupitia benki..
- (ii) Mwanafunzi alete 'Original Bank Payment slips' shuleni ili apate stakabadhi toka msarifu wa shule.

5.0 **MAHITAJI YA LAZIMA ANAYOTAKIWA KUYALETA.**

5.1 **KARO [SCHOOL FEES]**

Karo ni **T.Shs.70,000/=** kwa mwaka. Unaweza kulipa karo yote kwa wakati mmoja [mwanzoni mwa muhula] au nusu (**T.Shs.35,000/=**)

5.2 **SARE YA SHULE [SCHOOL UNIFORM]**

1. Mashati mawili (2) meupe, mikono mirefu, yasiyo na maridadi, yasiyoonyesha (Non-transparent) na yasiyobana yanapatikana shuleni. @ **T.Shs 12,000/=JUMLA 24,000/=.**
2. Sketi mbili zinashonwa shuleni kwa gharama ya T.Shs. **15,000/= @. JUMLA 30,000/=.** Sketi zitakazoshonwa mahali pengine hazitakubalika.
3. Sweta linapatikana shuleni kwa gharama ya **T.Shs.15,000/=.**
4. Tai inapatika shuleni kwa gharama ya **T.Shs.3,500/=.**

5. Nembo kwenye Mashati yanachapishwa shuleni kwa gharama ya **T.Shs.2,000/=**
6. Kitambulisho **T.Shs.5000/=**Kitaandaliwa shuleni.
7. T-shirt ya shule **T.Shs.15,000/=**
8. Vazi la kushindia (gauni) litashonewa shuleni kwa gharama ya **T.Shs. 20,000/=**
9. Stockings (Soksi ndefu) nyeupe jozi mbili (2).zisizo na urembo zinapatikana shulenikwa gharama ya **T.Shs.6,000/= kwa jozi mbili**
10. Viatu vyeusi vya ngozi vya kufunika (**Ajinunulie**). Viatu vyenye visigino virefu ama visivyo na soli ama vya plastiki havitakiwi.Atakaekiuka atachukuliwa hatua za kinidhamu.

Katika kukamilisha sare ya shule, **nywele lazima ziwe fupi** za kuchana,kucha ziwe fupi na zisipakwe rangi na uvaaji wa mapambo ni **marufuku**.

Kumbuka: *Uje umevaa sare za shule uliyokotoka na utaitumia kabla ya kupewa sare za shule hii.*

JUMLA ni T.sh.120,500/=

5.3 MALIPO MENGINE:

1. Fedha za tahadhari (Caution Money) ni **Tshs.20, 000/=**.Fedha hizi hulipwa mara moja kwa miaka miwili
2. Ulinzi **T.Shs.20,000/=**kwa mwaka.
3. Taaluma **T.Shs.30,000/=**. Kwa mwaka
4. Kiti na meza **T.Shs. 60,000/=** .Kwa miaka miwili.
5. Ujenzi wa ukuta **T.Shs.70,000/=**.Hulipwa mara moja tu mwanafunzi anapoingia shule.
6. Matibabu **T.Shs.30,000/=** kwa mwaka.
7. Godoro la sponji lenye ukubwa wa futi 2½ linapatikana shuleni hapa kwa kukodisha kwa shilingi elfu thelathini tu (**T.Shs.30,000/=**) kwa miaka miwili .Hivyo usije na godoro.

JUMLA ni T.sh. 260,000/=

ADA inalipiwa kwenye A/C **42710006674 NMB**
 Michango mingine kwenye A/C **42710006675 NMB**
 JINA la A/C zote ni **ARUSHA GIRLS HIGH SCHOOL**

Nyuma ya slip ya benk andika jina la mwanafunzi.

5:4 MAHITAJI MENGINE

1. Rimu mbili Photocopy paper size A4.
2. Jembe na reki au jembe na kwanja ama fedha tasilimu /cash zinazotosha kununua vifaa hivyo.
3. Jalada (file cover) moja (1) rangi ya kaki.

5:5

MAHITAJI BINAFSI YA MWANAFUNZI

1. Mathematical set, calculator ,graf pad na kalamu za wino/ball pen za kumtosha,penseli na vifaa vingine vya kujifunzia.
2. Madaftari ya kutosha masomo yake.
3. Begi/Mfuko mzuri wa kuweka vifaa vya darasani.

5:6

MAHITAJI YA MALAZI YA BWENI

- [i] Track suit rangi ya blue bahari au dark blue
- [ii] Chandarua ya rangi nyeupe
- [iii] Shuka rangi ya pink nne (4)
- [vi] Mablanke mawili (2)
- [v] Mto na foronya nyeupe/pink (2)
- [vi] Nguo za kulalia (Night Dress/pyjamas)
- [vii] Sanduku imara la bati la kuhifadha mali yako. Tunapokea sanduku moja tu.
- [viii] Taulo moja na kanga/vitenge doti moja.
- [ix] Mahitaji yote ya bafu e.g. sabuni, mafuta, dawa ya meno.
- [x] Ndoo moja ya kuogea na chombo cha kuhifadha maji safi ya kunywa.
- [xi] Tochi 1 na betri zake.

5:7

MAHITAJI YA 'DINING HALL'

- | | | | |
|------|--------|-------|---------|
| (i) | Sahani | (iv) | Kikombe |
| (ii) | Bakuli | (iii) | Kijiko |

5:8

MAHITAJI YA MICHEZO:

1. Bukta moja rangi ya blue (blue sky)
2. Sketi fupi (nap round) ya blue
3. T-shirt nyeupe
4. Raba nyeusi
5. Soksi nyeupe

Utakapofika shuleni utasomewa/utapewa sheria/kanuni za shule na utaratibu mzima wa shule hii na utalazimika kufuata. Ukikosa utaonywa na kuadhibiwa na ikilazimu utafukuzwa shule.

MWISHO, NATUMIA TENA NAFASI HII KUKUKARIBISHA HAPA SHULENI "ARUSHA GIRLS HIGH SCHOOL" NA NI MATARAJIO YANGU KUWA UFIKAPO HAPA UTATUMIA VEMA NAFASI HII ULİYOTUNUKIWA NA TAIFA.

Kumbuka*

Kama hujaripoti shuleni hadi ifikapo tarehe 30/8/2015 utahesabiwa kuwa umeikataa nafasi hii, hivyo itachukuliwa na mwanafunzi mwingine.

Mwanafunzi hataruhusiwa kuingia darasani bila kulipa ada na michango mingine yote. Hakikisha unatimiza mahitaji yote kuepuka usumbufu usio wa lazima.

**OFISI YA WAZIRI MKUU
TAWALA ZA MIKIOA NA SERIKALI ZA MITAA**

ARUSHA GIRLS HIGH SCHOOL

SHERIA ZA SHULE

Lengo la sheria za shule yetu ni kumjenga mwanafunzi kuwa na mwenendo mzuri kitabia hivyo kumwezesha kufaniwa kupata kile ananostahili haswa taaluma. Sheria hizi zitasaidia kuleta hali ya **AMANI, UMOJA** na **FURAHA** shuleni na kumfanya kuwa raia mwema . Kila mwanafunzi aje na nia ya **KUSOMA KWA BIDII, KUJITUMA** na ajitahidi kuishi vizuri katika jumuiya ya shule hii na majirani zetu pia

Kwa upande wa shule sisi **WALIMU** pamoja na **WAFANYAKAZI WASIO WALIMU** tutajitahidi kuishi, kumfundisha na kumlea mtoto katika maadili mema lakini tutashindwa katika kazi hii bila ushirikiano mzuri wa wazazi/walezi.

Vifuatavyo ni vifungu muhimu vya sheria za shule. Kila mmoja anatakiwa kuzifuata kwa ukamilifu.

- i. Kuheshimu bendera ya Taifa, picha za viongozi wa serikali, Nembo ya Taifa “**coat of Arms**” wimbo wa Taifa na fedha za Taifa.
- ii. Lugha inayotumika darasani na nje ya darasa ni Kiingereza tu. Hii inasaidia kuleta ufanisi katika masomo.
- iii. Kwa vile shule ni mahali pa kusoma inatakiwa pawe na ukimya hasa sehemu za madarasani na sehemu nyingine za kujifunzia.
- iv. Kila mwanafunzi ni lazima ahudhurie vipindi vyote vinavyompasa kama Ratiba ya Shule inavyoonesha. Kazi za mikono ni sehemu ya elimu inayotolewa hapa shuleni. Kila mmoja lazima ashiriki kikamilifu bila utegaji.
- v. Hairuhusiwi kupeleka chakula nje ya bwalo la chakula kama bwenini.
- vi. Mwanafunzi haruhusiwi kukaa na dawa za aina yoyote. Mwanafunzi anapolazimika kuwa na dawa atoe taarifa kwa matroni ili aweze kuhifadhiwa. Wanafunzi hawaruhusiwi kupeana dawa (Bweni).
- vii. Wanafunzi hawaruhusiwi kuongea na mgeni yeyote bila ruhusa ya Mkuu wa Shule/makamu mkuu wa shule/mwalimu wa zamu
- viii. Wizi, matusi au ugomvi haviruhusiwi kabisa hapa shuleni. Mwanafunzi atasimamishwa masomo akipatikana na makosa haya.
- ix. Kupata, kutoa mimba ni mambo ambayo shule hii haitegemei kwa vile kila msichana mwema anamcha Mungu na ana malengo mazuri katika maisha yake na atakaebainika atafukuzwa shule.
- x. Mwanafunzi hauruhusiwi kuja na vyombo vya muziki kama **radio, kanda (walkman, earphones), camera** na **simu za mkononi**.

NIMARUFUKU MWANAFUNZI KUWA NA SIMU SHULENI. AKIPATIKANA NAYO ATANYANG'ANYWA NA ITAHARIBIWA KABISA. AKIRUDIA TENA ATAFUKUZWA SHULE.

- xi. Kila mmoja anawajibika kuvitunza kwa uangalifu wa hali ya juu vifaa vyote vya shule atakavyokabidhiwa na asivyokabidhiwa. Uharibifu wowote utakaotokea gharama za matengenezo zitalipwa na atakayehusika na uharibifu huo. Mfano, Kuvunja vioo vya madirisha, milango n.k.
- xii. Kila Ijumaa na Jumapili wale waendao kusali kwenye madhehebu mabalimbali lazima warudi shuleni mara tu baada ya sala zao kumalizika, wawahi kurudi na kuendelea na ratiba ya shule watatoka na sare za shule (Uniform).

MIPAKA YA SHULE:

- xiii. Ni marufuku mwanafunzi kwenda kwenye nyumba za walimu/wafanyakazi bila kibali.
- xiv. Ni marufuku kuingia au kutoka shuleni bila ya sare ya shule hii ni pamoja na wakati wa kwenda likizo na kutoka likizo.

KILA MWANAFUNZI ANATEGEMEWA KUWA NA HESHIMA KWA WATU WOTE HAPA SHULENI NA KWA WAGENI ATUMIE LUGHA SAFI WAKATI WOTE NA AELEZE MATATIZO YAKE KWA VIONGOZI WANAOHUSIKA AWATII VIONGOZI WOTE NA ASHIRIKIANE NA WENZAKE KWA UPENDO, HESHIMA, AMANI NA UNDUGU:

R.S.JUMA
MKUU WA SHULE
SIMU NA. 0784 793422 /0757 792655

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
OFISI YA WAZIRI MKUU
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

FOMU YA UTII NA TABIA NJEMA

Mimi -----(jina kamili)

Kidato cha ----- mwaka -----

Natambua wajibu wangu kwa Taifa kama mwanafunzi na naahidi:-

- (a) Kwamba nitatii na kuwaheshimu viongozi wangu wote kuanzia ngazi ya darasa, viranja, walimu, watumishi wote hadi Mkuu wa Shule.
- (b) Kwamba nitafuata sheria na kanuni zote za shule pamoja na maelekezo yote yanayotolewa mara kwa mara na uongozi wa shule.
- (c) Kwamba sitatoka nje ya mipaka ya shule wakati wa masomo labda tu kwa shughuli maalumu na baada ya kupata kibali maalumu kutoka kwa Mwalimu au Mkuu wa Shule mwenyewe.
- (d) Kwamba kama nitashindwa kufuata hayo yote hapo juu, hatua kali ichukuliwe dhidi yangu ambayo ni pamoja na kusimamishwa masomo.

Tarehe -----

Jina na Sahihi ya Mwanafunzi

Tarehe -----

Jina na Sahihi ya Shahidi Mzazi/Mlezi

Tarehe -----

Sahihi ya Mkuu wa Shule

SHULE YA SEKONDARI YA WASICHANA ARUSHA

FOMU YA KUJIANDIKISHA SHULENI

HABARI ZA MZAZI/MLEZI

1. Jina kamili la Baba -----
2. Kazi yake -----
3. Jina kamili la Mama -----
4. Kazi yake -----
5. Jina kamili la Mlezi (iwapo mtoto haishi na wazazi wake)

6. Kazi na Anwani ya Mzazi/ Mlezi -----

7. Nyumbani kwa baba (alipozaliwa mtoto) au 'Place of Domicile'
Kijiji/Mtaa ----- Wilaya -----
Kata ----- Mkoa -----
Tarafa -----
8. Anwani ya mahali pa kazi ya baba -----

Nambari ya simu -----
9. Anwani ya mahali pa kazi ya mama -----
Nambari ya simu -----
10. Mtoto anaishi na (i) Baba tu (ii) Mama tu (iii) Wazazi wote
(iv) Walezi ***Kata isiyohusika***
11. Dini ya Baba ----- Dhehebu -----
Dini ya Mama ----- Dhehebu -----Dhehebu
unalotaka mwanao alelewe -----
12. Anwani kamili ya nyumba ambapo mtoto atakuwa anakwenda siku za likizo: -----

13. Mimi ----- (Baba/Mama/Mlezi wa -----
----- Nathibitisha kuwa taarifa hiyo hapo juu ni sahihi na haahidi
kushirikiana na walimu ili kuhakikisha kwamba kijana wangu anakuwa na tabia nzuri, mchapa
kazi na mwenye bidii ya masomo.

Tarehe -----

-----Jina na sahihi ya
Mzazi/Mlezi

**OFISI YA WAZIRI MKUU
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

FOMU YA KUKUBALI NAFASI NA UTII

Mimi -----(jina kamili)

Kidato cha ----- mwaka -----

Nakubali na nahaidi kufuata sheria na taratibu za Shule kama zilivyopangwa. Nikienda kinyume nichukuliwe hatua za kinidhamu.

Tarehe -----
Jina na Sahihi ya Mwanafunzi

Tarehe -----
Sahihi ya Mkuu wa Shule

Mimi Mzazi/Mlezi wa ----- nimesoma na kuelewa/kukubaliana na sheria na kanuni za shule. Endapo mtoto wangu atashindwa kufuata hayo yote hatua kali dhidi yake zichukuliwe ikiwa ni pamoja na kusimamishwa masomo.

Tarehe ----- Jina na Sahihi ya Mzazi/Mlezi -----

Tarehe ----- Jina na Sahihi ya Shahidi -----

Tarehe ----- Sahihi ya Mkuu wa Shule -----

6.0. VITABU

Ifuatayo ni baadhi ya orodha ya vitabu vinavyotumika darasani. Wanafunzi wajitahidi kuwanavyo angalau vichache.

ECONOMICS:

- Text Book of Economics by J.L. HANSON
- Economic Simplified by SALEEMI
- Modern economic' by KHAN.
- Macro economic Theory by M.L JHINGAN
- Micro Economic Theory by M.L JHINGAN
- Introductory Economics by STANLAKE'S

GEOGRAPHY:

- Landforms in Africa by COLIN BUCKLE.
- Principles of Physical Geography by MONKHOUSE.
- Geography. Integrated Approach by WAUGH.
- Practical Geography for Africa by J.M. PRITCHARD.
- AFRICA by J.M. PRITCHARD.
- Tropical Lands by MICHAEL SENIOR.
- Human and Economic geography by MORGAN.

MATHEMATICS:

- Pure Mathematics by K.J. BACKHOUSE
- Advanced level Math's Vol. 1 by L.K. SHAYO.
- Modern ABC.
- Advanced Level Pure Mathematics, fourth Edition by C.J TRANTA

PHYSICS:

- Principle of physics XI by Chand
- Principle of physics XII by Chand
- Understanding Physics by Jim Breclhaupt
- Objective of Physics by Chand
- Advance Physics by Roger Munchester
- Physics by Tom Duncan
- Calculation for A Level physics
- Physics ABBOT

THE PRIME MINISTERS OFFICE
REGIONAL ADMINSTRATIONS AND LOCAL GOVERNMENT

ArushaGirls High School,
P.O.Box. 16034,

ARUSHA

Ref. AGHS / F.V 2015

Date:

REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION

PART A:

Ref. No:

Medical Officer

Date: -----

RE: -----

FORM 5 -----

Please examine the above named as to her fitness for admission as a student of this school.

Thank you.

R.S.JUMA
HEADMISTRESS
MOBILE NO.. 0784 793422 /0757 792655

PART B:

MEDICAL CERTIFICATE

(To be completed by a Medical Officer)

I have examined the above named student and consider that he/she is fit/not fit for studies:

Explanation if any -----

Date -----

Signature -----

Station: -----

Designation -----